**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAWASILIANO, TEKNOLOJIA YA HABARI NA UBUNIFU


**ILIYOWASILISHWA NA**

**MHESHIMIWA MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM).**

**WAZIRI WA MAWASILIANO, TEKNOLOJIA YA HABARI NA UBUNIFU**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**JUNI, 2026**


VIONGOZI WA WIZARA
Naibu Waziri wa Mawasiliano
Teknolojia ya Habari na Ubunifu
WAKUU WA TAASISI CHINI YA WIZARA
ZICTIA

**YALIYOMO**

YALIYOMO ................................................ ii
ORODHA YA VIAMBATISHO ................................................ v
A.UTANGULIZI ................................................ 1
MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA ................................................ 3
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ................................................ 4
B. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ................................................ 4
C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026 ................................................ 6
MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ................................................ 6
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KUU NA PROGRAMU NDOGO ....... 9
PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) ................................................ 9
PROGRAMU NDOGO YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEHAMA ................................................ 10
HALI YA UPATIKANAJI MAWASILIANO ZANZIBAR ........................ 11
D. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWANA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 ... 14
SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR (ZICTIA) ........................... 14
UTEKELEZAJI WA MALENGO YA SHIRIKA KWA MWAKA WA FEDHA2025/2026 ................................................ 15
MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA SHIRIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2025 – 2026 ................................................ 17
MAPATO NA MATUMIZI ................................................ 20
MAPATO ................................................ 20
MATUMIZI ................................................ 20
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR (EGAZ) ................. 20
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ......................... 22
PROGRAMU KUU YA HUDUMA ZA SERIKALI MTANDAO .............. 22
PROGRAMU NDOGO YA MIUNDOMBINU NA MIFUMO YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO ................................ 22

PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO ........ 24
PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI WA SERIKALI MTANDAO....... 28
PROGRAMU NDOGO YA UENDESHAJI, UTUMISHI NA MIPANGO. 28
MUHTASARI WA TAARIFA YA UPATIKANAJI WA FEDHA .............. 31
PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SERIKALI MTANDAO PEMBA. ........ 32
E. MUELEKEO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027........ 35
SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR (ZICTIA) ........ 35
MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ..... 36
MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO ........ 36
MAKADIRIO YA MATUMIZI ........ 36
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR (EGAZ)........ 36
F. MWELEKEO WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ........ 38
PROGRAMU ZINAZOSIMAMIWA NA KUTEKELEZWA NA WIZARA YA MAWASILIANO, TEKNOLOJIA YA HABARI NA UBUNIFU KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027......... 40
MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ........ 40
PROGRAMU KUU YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI (TEHAMA)........ 41
PROGRAMU NDOGO YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA TEHAMA ........ 41
IDARA YA MAWASILIANO NA MIUNDOMBINU ........ 41
PROGRAMU NDOGO YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI NA UBUNIFU KATIKA TEHAMA. ........ 42
IDARA YA USALAMA MTANDAO NA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI. 42
IDARA YA UBUNIFU ........ 43
PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA. .... 44
PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA UTAWALA NA UENDESHAJI ........ 44
IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI ........ 44

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA........................................................ 45
IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI ........................................ 45
PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA ........................................................................................ 46
OFISI KUU PEMBA ........................................................................ 47
PROGRAMU KUU YA UENDELEZAJI WA MIFUMO YA MAWASILIANO ZANZIBAR ........................................................................................ 47
MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI NA UBUNIFU KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ........................... 48
MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA ............................................... 48
MATUMIZI YA MIRADI YA MAENDELEO ....................................... 49
SHUKURANI NA HITIMISHO ......................................................... 49
SHUKURANI .................................................................................. 49
HITIMISHO .................................................................................... 52
G. VIAMBATISHO ......................................................................... 53

**ORODHA YA VIAMBATISHO**

Kiambatisho Nambari 1A:Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Kwa Programu Kwa Kipindi cha Julai, 2026 hadi Machi,2026 ........................................................... 54
Kiambatisho Nambari 1B:Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Kwa Programu Kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ........................................................ 55
Kiambatisho Namabari 2:Orodha ya Maeneo na Kampuni iliyojenga Minara ........................................................ 57
Kimbatanisho Nambari 3:Minara ya Simu kwa aina ya teknoljia ya urushaji wa mawimbi (2G, 3G, 4G na 5G) kwa mikoa ya Zanzibar ...................................................... 59
Kiambatisho Nambari 4:Mgawanyo wa Minara ya Simu kwa Kila Mkoa ............................................................... 60
Kiambatisho Nambari 5:Idadi ya laini za simu kwa Mikoa ya Zanzibar ................................................................ 61
Kiambatisho Nambari 6:Kuunganisha Taasisi za Umma na Mtandao wa Serikali (Government Network Connectivity) ... 62
Kiambatisho Nambari 7:Mgawanyiko wa Mapato ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2026/2027 .... 63
Kiambatisho Nambari 8:Mchanganuo wa fedha za Matumizi ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 .......................................................... 64

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwa Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili lipokee na kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu kwa kazi za kawaida na kazi za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia afya njema na kutukutanisha tena katika kikao hiki tukiwa katika hali ya uzima na afya njema. Aidha, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uwezo wa kuendelea na majukumu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar katika hali ya amani na Utulivu katika nchi yetu.

3. **Mheshimiwa Spika**, Kwa heshima kubwa, napenda kutoa pongezi kwa Marais Wetu wapendwa; Dkt Samia Suluhu Hassan na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuaminiwa na kupewa ridhaa na wananchi kuendelea kuwatumikia katika kipindi cha pili cha awamu zao wananchi wana matumaini makubwa kwa serikali kupitia ahadi zilizotolewa wakati wa kuinadi ilani ya Chama Tawala - CCM ya mwaka 2025 -2030 kupitia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba mwaka 2025. Hii inatokana na kusimamia utekelezaji wa uhakika wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima naomba kutumia fursa hii kipekee kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uamuzi wake wa busara wa kuanzisha Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu tarehe 13, Novemba, 2025. Aidha, napenda kumshukuru kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa kwanza wa Mawasiliano,Teknolojia ya Habari na Ubunifu.

Ninamuahidi kuwa nitatekeleza majukumu aliyonikabidhi ya kusimamia Sekta ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu kwa juhudi, maarifa na uadilifu ili kuiwezesha Zanzibar kuenda katika Mageuzi ya Kidijitali na kufikia azma ya kuwa na Uchumi wa Kidijitali.

5. **Mheshimiwa Spika,** vilevile nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa umahiri wake katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia, kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kuratibu shughuli zote za Baraza la Wawakilishi. Namshukuru kwa maelekezo na ushauri wake anaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza Sekta hii muhimu kwa Maendeleo ya Zanzibar.

6. **Mheshimiwa Spika,** napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kwa mara nyingine kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi. Kuaminiwa huku kunatokana na kuliongoza Baraza hili kwa weledi, busara na hekima nyingi. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi na Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Dimani kwa kuongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Baraza la Wawakilishi. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Hudhaima Mbarak Tahir na Dkt. Mahmoud Omar Hamad kwa kazi wanayoifanya ya kukusaidia kuliongoza Baraza lako Tukufu kwa kusimamia shughuli za Baraza kwa maslahi ya Wananchi na Taifa kwa ujumla. Vile vile, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kazi wanazozifanya za kusimamia utekelezaji wa Wizara na Sekta za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

7. **Mheshimiwa Spika,** aidha, naipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA ya Baraza la

Wawakilishi inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mihayo Juma Nhunga, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mwera, Makamo Mwenyekiti wa Kamati na Mwakilishi wa Viti Maalum Wanawake, Mheshimiwa Mwanaidi Kassim Mussa na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wao kwangu na Wizara ya Mwasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu kwa ujumla katika kuhakikisha malengo ya Sekta yanafikiwa. Aidha, ninaishukuru Kamati kwa kujadilili na kupitisha kwa kauli moja Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu (Fungu 059), kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

8. **Mheshimiwa Spika,** nitakuwa mwizi wa fadhila nisipompongeza na kumshukuru Ndugu Raya Issa Mselem, Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa utendaji wake bora na mashirikiano anayonipa yeye binafsi na Watendaji wengine wote wa Baraza la Wawakilishi.

9. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kulitumikia taifa. Vilevile, naomba kuwashukuru Wapiga Kura wa Jimbo la Uchaguzi la Bububu kwa kuniamini na kunichagua kuwawakilisha katika Baraza hili. Nawaomba waendelee kunipa ushirikiano katika kuliletea maendeleo Jimbo letu.

## MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na ubunifu ina majukumu ya Kuandaa, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera zinazohusu Mawasiliano, Teknolojia ya Habari (TEHAMA) na Ubunifu; Kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Sera, Mipango na Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Serikali kwa wananchi; Kufanya tafiti za maendeleo na ubunifu kwenye TEHAMA; Kuendeleza wataalam wa TEHAMA; Kusimamia ujenzi na uendeshaji

wa Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano; Kusimamia ulinzi na usalama wa mtandao; Kuboresha na kuendeleza utendaji wa rasilimali watu ndani ya Wizara, Kusimamia na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za Serikali na Kusimamia Taasisi, Programu na Miradi ndani ya Wizara. Majukumu hayo yana lengo la kusimamia Mageuzi ya Kidijitali ambayo yataipeleka Zanzibar katika Uchumi Jumuishi wa Kidijitali.

**11.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu inatekeleza majukumu hayo kupitia Idara tano (5), Ofisi Kuu Pemba na Taasisi mbili (2). Idara zinazosimamiwa na Wizara ni: Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Mawasiliano na Miundombinu, Idara ya Usalama Mtandao na Ulinzi wa Taarifa na Idara ya Ubunifu. Taasisi zinazosimamiwa na Wizara ni Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ).

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### B. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKAWA FEDHA 2025/2026

**12.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara pamoja na Taasisi zake ziliandaa mpango wake wa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025; Ahadi na Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050; Mpango wa Taifa wa Maendeleo Zanzibar – ZADEP (2021 – 2026) na Sera ya TEHAMA ya Zanzibar ya mwaka 2013. Aidha, Wizara ilizingatia Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

13. **Mhashimiwa Mwenyekiti,** kwa kuzingatia Miongozo hiyo, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu ilijikita katika utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo:

a. Kuendelea kuimarisha mifumo ya Mawasiliano Zanzibar kwa kuimarisha Miundombinu ya Mkonga, kutengeneza mifumo mbalimbali ya kidijitali pamoja na kuandaa Master Plan ya Cyber City;
b. Kuanza mradi wa kulaza Mkonga wa Kimataifa wa baharini (International Gateway);
c. Kuanza ujenzi wa Kituo Mbadala cha Kuhifadhia Taarifa (Data Center);
d. Kuimarisha huduma za mtandao katika maeneo ya umma (Public Wi-Fi);
e. Kutayarisha Miongozo ya Mageuzi ya Kidijitali pamoja na kutunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Faragha na Kampuni Chipukizi (Startups);
f. Kuweka mazingira wezeshi kwa kuimarisha Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na kuvutia wawekezaji kwa kuweka Sera, Sheria na Kanuni ambazo zinaendana na mazingira ya Kitaifa na Kimataifa;
g. Kuboresha Mfumo wa Anuani za Makaazi Zanzibar pamoja na kuwapatia wananchi uelewa wa matumizi ya Mfumo huo;
h. Kuendelea kuwajengea uwezo wananchi 2,500 kwa kuwapatia mafunzo ya kidijitali kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii, kuboresha na kuanzisha Vituo vipya katika maeneo tofauti;
i. Kujenga na kusimamia Kituo cha Ubunifu na Ujasiriamali katika Sekta ya TEHAMA kwa lengo la kuwajengea uwezo vijana, kuibua vipaji na kuongeza Soko la Ajira kupitia TEHAMA;
j. Kujenga uelewa wa matumizi ya TEHAMA kwa makundi maalum na wenye mahitaji maalum;
k. Kuimarisha Mifumo ya ukusanyaji wa mapato;

l. Kukamilisha Kanuni za Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao;
m. Kuimarisha miundombinu ya pamoja ya Serikali;
n. Kuongeza usalama wa mifumo yote ya Serikali;
o. Kufanya mapitio na kuhuisha sera, miongozo, na viwango vya TEHAMA; na
p. Kusimamia miradi ya TEHAMA kutoka katika Taasisi za Umma

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026

### Mafanikio na Changamoto

**14. Mheshimiwa Spika,** kabla ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa Program Kuu na Programu Ndogo za Wizara kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, naomba kuwasilisha mafanikio yaliyopatikana pamoja na changamoto zilizojitokeza. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Sekta ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu tumefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

a. Kutunga Rasimu ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2026 (the Personal Data Protection Act, 2026).
b. Kugawa Vishkwambi kwa Wizara, Mikoa, Manispaa, Mabaraza ya Miji, Halmashauri na Masheha wote wa Unguja na Pemba, kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji na uhakiki wa taarifa za Anuani za Makaazi pamoja na kutumia vishkwambi hivyo katika kutoa huduma za Serikali kwa njia ya kidijitali. Jumla ya Vishkwambi 409 vimetolewa kwa ajili ya kufanikisha kazi hizo.
c. Kutoa huduma ya Barua ya Utambulisho kwa njia ya Kidijitali kwa kutumia Mfumo wa Anuani za Makaazi, ambapo jumla ya barua 29,475 zimetolewa katika Shehia za Unguja na Pemba.
d. Kuboresha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano ya katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba yakiwemo

maeneo ya Visiwa Vidogo Vidogo. Jumla ya Minara ya Mawasiliano 27 imeruhusiwa kujengwa na Makampuni ya Ujenzi wa Minara.

e. Kuwezesha elimu ya TEHAMA na Dijitali kwa umma. Wizara kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii imetoa mafunzo kwa wananchi 1,015, kati yao wanawake ni 639 na wanaume ni 376.
f. Kuwekeza katika Mfumo wa Mkonga wa Taifa na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika miundombinu ya kidijitali. Wizara kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidigitali imefanikiwa kupeleka Mkonga wa Mawasiliano katika Vituo vya Unguja na Pemba ambapo jumla ya vituo 153 kati ya 211 vimepelekewa Mkonga wa Taifa wa mawasiliano sawa na asilimia 72.51 ya utekelezaji. Kati ya vituo hivyo, vituo 101 viko Unguja na vituo 52 viko Pemba.
g. Kuimarisha Sekta ya Ubunifu na Kuongeza Thamani ya Bidhaa za Utamaduni. Wizara imefanikiwa kuwasajili wabunifu kumi na tisa (19) pamoja na kuwapa elimu na maelekezo ya kuviendeleza vipaji vyao ili waweze kupata fursa za matamasha ya Kitaifa na Kimataifa na kuongeza wataalamu katika Sekta husika;
h. Wizara imefanikiwa kutunga Sera ya Kidijitali ya Zanzibar ya mwaka 2026 (the Zanzibar Digital Policy, 2026) na imeshakamalika ambayo inatokana na mapitio ya Sera ya TEHAMA ya Zanzibar ya mwaka 2013 (the Zanzibar ICT Policy, 2013).
i. Wizara imeanza mchakato wa kutunga Sheria ya Kampuni Chipukizi (the Startup and Innovation Act) kwa kushirikiana na Chama cha Umoja wa Kampuni Chipukizi Zanzibar (Zanzibar Startup Association - ZSA) pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (United Nations Development Program – UNDP).
j. Kuendeleza kwa mifumo ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mapato ya TEHAMA. Miongoni mwa mifumo hiyo ni:

- ZanMalipo - Mfumo wa Ukusanyaji Mapato ya Serikali,
- e-Proz - Mfumo wa Manunuzi Serikalini,
- BAMAS - Mfumo wa Bajeti na Matumizi Serikalini,
- ERMS - Mfumo wa Uendeshaji na fedha kwa Taasisi zinazojitegemea pamoja na kuziwezesha Taasisi kuwa na Mifumo ya Malipo (Billing System).

k. Mifumo ya Uwazi na uwajibikaji katika utendaji wa Serikali ambayo ni:-
   - e-Office (Mfumo wa Masjala Mtandao),
   - Mfumo wa barua pepe (GMS),
   - ZanVibali (Mfumo wa Kuomba ruhusa ya Safari nje ya Nchi),
   - ZanAjira (Mfumo wa Uajiri Serikalini)
   - Mfumo wa ICT Register
   - Mfumo HR Payroll pamoja na
   - Mfumo wa e-Saini.

l. Uandaaji wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao
   - Imeratibu uandaaji wa miongozo na viwango vya TEHAMA vinavyotumika serikalini. Miongozo hii imeimarisha usimamizi wa matumizi ya TEHAMA, utengenezaji wa mifumo pamoja na ununuzi wa vifaa. Vile vile imeanzisha sera ya usalama wa taarifa na taratibu za uidhinishaji wa data pamoja na uwekaji wa Miundombinu ya kuhifadhi taarifa kwa usalama.

**15. Mheshimiwa Spika,** wakati wa utekelezaji wa majukumu ambayo yamepelekea kupata mafanikio yaliyotajwa changamoto kadhaa zilijitokeza ambazo ni pamoja na:

a. Kukosekana kwa fedha zilizopangwa kutekeleza shughuli za uendeshaji na miradi ya maendeleo, ambapo imepelekea Miradi hiyo kutotekelezwa kwa ufanisi. Katika kukabiliana na changamoto hii Wizara imetekeleza shughuli zote ambazo hazihitaji rasilimali fedha kama vile kuandaa nyaraka za kutafuta wakandarasi, hadidu za rejea (TOR) pamoja na kutafuta njia mbadala ya utekelezaji wa Miradi hiyo kwa kushirikiana na Sekta binafsi (PPP);

b. Uchakavu wa miundombinu ya Vituo vya TEHAMA Jamii pamoja na Vifaa vilivyomo ambavyo hutumiwa na wananchi katika kupata elimu ya kidijitali;
c. Ongezeko la vitisho vya usalama wa mifumo ya TEHAMA; Kutokana na kukua kwa matumizi ya mifumo ya kidijitali, kumekuwa na ongezeko la vitisho vya kiusalama mtandaoni (Cyber Attacks) vinavyohitaji uwekezaji mkubwa katika mifumo ya usalama wa taarifa na miundombinu ya TEHAMA; na
d. Kuchelewa kwa malipo au kutokulipwa kabisa kwa huduma za mawasiliano (Mtandao), na matumizi ya mkonga kwa Taasisi za Serikali hii inapelekea Shirika kutokufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato.

**Utekelezaji wa Programu Kuu na Programu Ndogo**

**16. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu imetekeleza kazi zake kupitia Programu Kuu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Programu hii ina Programu Ndogo moja ambayo ni "Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA".

**Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**17. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu hii ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 77,721,217,485** kwa mshahara, kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 379,914,000** ni mshahara, **Shilingi 1,290,403,485** ni kazi za kawaida na **Shilingi 76,050,900,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Programu hii ilipangiwa kutumia **Shilingi 62,481,796,894**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 284,935,500** ni mshahara, **Shilingi 545,961,394** ni kazi za kawaida na **Shilingi 61,650,900,000** ni kwa ajili

ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **Shilingi 800,820,269** zimetumika sawa na asilimia 1.3 ya makadirio ya bajeti kwa kipindi cha miezi tisa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 216,394,950** ni mshahara sawa na asilimia **76**, ya makadirio ya miezi tisa, **Shilingi 584,425,319** ni kazi za kawaida sawa na asilimia **107** kwa kipindi cha miezi tisa. Kwa upande wa miradi ya maendeleo hakuna fedha iliyopatikana hadi kufikia Machi 2026. Aidha, mabadiliko ya fedha zilizotengwa kwa upande wa kazi za kawaida yametokana na mgao wa fedha (reallocation) zilizohamishwa na Wizara ya Fedha na Mipango kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwenda Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa shughuli za kiutawala na kiuendeshaji baada ya kuanzishwa Wizara hii. **Kiambatisho Nambari 1A.**

**Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA**

**18. Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kusimamia uwepo wa miundombinu na huduma bora za TEHAMA zilizo salama na endelevu kwa Zanzibar. Programu hii pia inasimamia upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu, mtandao (Internet) pamoja kusimamia maendeleo ya huduma za TEHAMA Zanzibar. Aidha, Programu hii inashajihisha Ubunifu na Uchumi wa Kidijitali kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji yanayotokana na uwekaji wa Sera na Sheria rafiki.

**19. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara kupitia Programu hii imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

a. **Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano:** Jumla ya Minara 27 imeruhusiwa kujengwa Zanzibar katika maeneo ambayo yameonekana kuwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano. Minara hiyo imejengwa kupitia

Makampuni yaliyopatiwa kibali Unguja na Pemba. Ujenzi wa Minara hii ni muendelezo wa juhudi za Serikali katika kuwasogezea wananchi huduma katika maeneo yao na kuhakikisha huduma za mawasiliano zinafikia asilimia mia moja katika maeneo yote ya Zanzibar. **Kiambatisho Nambari 2.**

**Hali ya Upatikanaji Mawasiliano Zanzibar**

Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kukua hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ambapo takwimuzinaoneshakuwaminarayamawasilianoimeongezeka kutoka minara 428 mwezi Machi, 2025 hadi kufikia minara 455 mwezi Disemba 2025 sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Kiambatisho 3 kinaonesha mgawanyo kwa kila mkoa. Aidha, mitambo ya utoaji wa mawimbi kwa teknolojia ya 2G, 3G, 4G na 5G imeongezeka kutoka mitambo 1,741 mwezi Machi, 2025 hadi kufikia mitambo 1,947 mwezi Machi 2026 sawa na ongezeko la asilimia 11.8. Kiambatisho 4 kinaonesha mgawanyo kwa kila mkoa. Takwimu hizo zimesababisha ongezeko la watumiaji wa mawasiliano ya simu ambapo laini za simu zilizosajiliwa Unguja na Pemba zimeongezeka kutoka 1,058,516 Mwezi Machi, 2025 hadi kufikia laini 1,310,668 Mwezi Machi, 2026 sawa na ongezeko la laini 252,152 amabayo ni sawa na asilimia 23.8. Mchanganuo wa laini zilizosajiliwa kwa kila Mkoa unaonekana katika **Kiambatisho Nambari 3, 4 na 5.**

b. **Kuunganisha Taasisi za Umma na Mtandao wa Serikali (Government Network Connectivity):** Kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania Project) Wizara imeunganisha na mkonga wa mawasiliano taasisi 153 kati ya Taasisi 211 za Serikali vikiwemo Vituo vya Afya na Skuli, ili kutoa huduma bora kwa wananchi wanaofika kupata huduma na kuwezesha Maendeleo ya Kidijitali. Kati ya taasisi hizo Unguja Taasisi 101 na Pemba Taasisi 52 tayari zimeshafikishiwa huduma hiyo. **Kiambatisho Nambari 6.**

c. **Utoaji wa Mafunzo ya TEHAMA kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii:** Wizara ilipanga kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa wananchi wapatao 2,500 hadi kufikia mwezi Machi, 2026 jumla ya wananchi 1,015 wamepewa mafunzo. Kati yao wanawake ni 639 na wanaume ni 376. Lengo la mfunzo haya ni kupunguza idadi ya wanajamii wasiojua kutumia Kompyuta na mitandao ili waweze kushiriki katika uchumi wa kidjitali.

d. **Utoaji wa Elimu na Uelewa Kuhusu Ulinzi na Usalama wa Mtandao:** Wizara imetoa elimu kwa Umma kuhusu Ulinzi na Usalama wa Mtandao kwa makundi mbalimbali ya Jamii ikiwa ni pamoja na Watumishi wa Umma, Masheha, waendesha bodaboda, maafisa TEHAMA wa Serikali na Wananchi kwa ujumla. Elimu hii imekuwa ikitolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo Redio, Televisheni, Mitandao ya Kijamii pamoja na kufanya vikao na mikutano.

e. **Kuweka mazingira wezeshi kwa kuimarisha sekta ya mawasiliano na Teknolojia ya Habari:** Wizara imetunga Sera ya Kidijitali ya Zanzibar ya mwaka 2026 (the Zanzibar Digital Policy, 2026) ambayo inatokana na mapitio ya Sera ya TEHAMA ya Zanzibar ya mwaka 2013 (the Zanzibar ICT Policy, 2013). Sera hii imeshakubaliwa na vikao vyote vya maamuzi vya Serikali, Wizara iko katika hatua za kuizindua rasmi sera hii na kufanya uelewa kwa wananchi.

f. **Kutunga Rasimu ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi:** Wizara tayari imeshaandaa rasimu ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambayo ni takwa la Kikanda na Kimataifa ili kuweza kulinda taarifa hizo kwa misingi ya Sheria pamoja na kuvutia wawekezaji. Rasimu ya Sheria hii tayari imepita katika Kikao cha Kamati ya Makatibu Wakuu na sasa iko katika hatua ya kupelekwa katika Kikao cha Baraza la Mapinduzi ili kupata maamuzi rasmi ya Serikali.

g. **Kuanza kwa utungaji wa Sheria ya Kampuni Chipukizi:** Wizara imeandaa Rasimu ya awali ya Sheria ya Kampuni Chipukizi (the Startup and Innovation Act) kwa kushirikiana

na Chama cha Umoja wa Kampuni Chipukizi Zanzibar (Zanzibar Startup Association - ZSA) Pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (United Nations Development Program – UNDP).

h. **Kufanya tathmini ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika Wizara na Taasisi za Serikali:** Wizara imefanya tathmini ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika Wizara 20 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), ikilenga kubaini hali ya sasa ya utendaji, usalama wa taarifa, uwezo wa uendeshaji pamoja na mapungufu yanayohitaji maboresho. Kwa ujumla, imebainika kuwa mifumo ipo katika hatua ya maendeleo lakini bado inahitaji maboresho ya kimkakati ili kuimarisha ufanisi, usalama na uthabiti wa utoaji wa huduma za Serikali. Tathmini imehusisha maeneo muhimu kama mifumo ya TEHAMA, miundombinu, usalama wa taarifa, na utekelezaji wa sera na kanuni, kwa kutumia mbinu za mahojiano, dodoso na mapitio ya kitaaluma.

   Matokeo yanaonesha uwepo wa changamoto mbalimbali ikiwemo udhaifu wa miundombinu ya mtandao, ukosefu wa usalama wa kutosha wa mifumo, kutounganishwa kwa mifumo mingi, uhifadhi duni wa taarifa pamoja na ukosefu wa sera na miongozo ya ndani ya TEHAMA. Aidha, upungufu wa wataalamu, bajeti ndogo, na ukosefu wa mafunzo endelevu umeathiri ufanisi wa utekelezaji wa TEHAMA. Kutokana na hali hiyo, mapendekezo yametolewa ikiwemo kuimarisha usalama wa mifumo, kuanzisha vituo vya pamoja vya usimamizi (kama SOC na SIEM), kuboresha miundombinu, kuwekeza katika rasilimali watu, na kuanzisha sera madhubuti za TEHAMA ili kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kwa njia ya kidijitali.

i. **Kusimamia na kuratibu Matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makaazi:** Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Anuani za Makaazi ambapo jumla ya anuani za makaazi 257 zimehakikiwa Unguja na Pemba. Aidha, huduma ya

utoaji wa barua za utambulisho wa wananchi kutoka kwa Sheha kwa njia ya kidijitali imeendelea kufanyika ambapo jumla ya barua za kidijitali 29,475 za wanafunzi wanaomba mikopo ya elimu ya juu zimetolewa. Huduma hii inaombwa bila kufika katika Ofisi za Shehia kwa kutumia Mfumo wa kidijitali wa Anuani za Makaazi (NaPA).

Vilevile, katika kufanikisha matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makaazi, Wizara imegawa Vishkwambi kwa Wizara, Mikoa, Manispaa, Mabaraza ya Miji, Halmashauri na Masheha wote wa Unguja na Pemba. Lengo ni kuwezesha ukusanyaji na uhakiki wa taarifa za Anuani za Makaazi pamoja na kutumia vishkwambi hivyo katika kutoa huduma za Serikali kwa njia ya kidijitali. Jumla ya Vishkwambi 409 vimetolewa kwa ajili ya kufanikisha kazi hizo pamoja na kufanya mafunzo ya uhamasishaji wa matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makaazi kwa Masheha wa Mikoa yote ya Unguja na Pemba. Matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makaazi yalizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar tarehe 16 Agosti, 2025.

## D.UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026

**20. Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza hapo awali kuwa, Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu inasimamia Taasisi mbili (2) ambazo ni Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) .

### Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA)

**21. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kupitia Sheria nambari 4 ya mwaka 2023 na limepewa jukumu la kusimamia na

kuendesha Miundombinu ya Kimkakati ya Mawasiliano ambayo ni Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wa Zanzibar na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhia Taarifa (Data Center).

**Utekelezaji wa Malengo ya shirika kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**22. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ZICTIA imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:

a. **Kuunganisha vituo vya Taasisi za Serikali na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano:** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 ZICTIA imefanikiwa kuviunganisha na mkonga jumla ya vituo kumi na Nne (14) vya Taasisi mbalimbali Unguja na Pemba ikiwemo Chuo cha Kiislamu – Maungani, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Wizara ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa upande wa Unguja.

   Kwa upande wa Pemba ni Tume ya Uchaguzi Zanzibar - ZEC, Shirika la Taifa la Biashara (Wete, Mkoani na Chake chake), Tume ya Ushindani Halali wa Biashara, Wakala wa usajili Mali na Biashara (BPRA) na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF).

b. **Maboresho ya Mkonga wa Mawasiliano:** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 ZICTIA imeendelea na maboresho ya Mkonga katika maeneo mbalimbali yenye urefu wa kilomita 290 Unguja na Pemba. Maboresho hayo yametokana na hitilafu ya uwekaji wa Miundombinu ya maji na Ujenzi wa Barabara. Kwa upande wa Unguja kazi hiyo imefanyika katika maeneo ya Sebleni, Tomondo, Fuoni, Chukwani, Kijichi, Kiwengwa, Magogoni, Maruhubi na Barabara ya Mkapa, Jambiani - Makunduchi, Tunguu - Pete, Tomondo - Kariakoo, Mbweni – Bandarini, Amani - Kwerekwe, Bumbwini - Mfenesini, Tunguu - Muyuni - Makunduchi na Pangatupu hadi Mahonda.

Aidha, kwa upande wa Pemba maboresho ya mkonga yamefanyika katika maeneo ya Mwambe, Micheweni, Kiwani, Pondeani, Mchangamdogo, Micheweni, Madungu, Wete, Mkoani, Kilindi, Pagali, Makangale, Kifumbikai, Mbuzini, Kinyasini, Pandani, Mchangamrima, Kipitacho Mkoani, Shungi, Tundauwa, Bungala, Vikunguni, Makangale, Fidel Castro, barabara ya Chake – Wete na barabara ya Chake - Vitongoji.

c. **Kuweka Njia Mpya (route) ya Mkonga wa Dharura:** Shirika la Mawasiliano limelazimika kuweka njia mpya ya Mkonga wa dharura katika maeneo mbalimbali ya Unguja kwa lengo la kunusuru kukosekana kwa mawasiliano itakayoweza kusababishwa na miradi ya ujenzi wa barabara inayoendelea nchini. Aidha, ZICTIA imeendelea na uimarishaji wa huduma katika vituo vya mkonga (POP) kwa kuvifanyia maboresho (services) na matengenezo ya vifaa mbali mbali ikiwemo vipoza hewa (AC) na Majenereta ya vituo vyote vya Unguja na Pemba.

d. **Kuhifadhi Taarifa za Mifumo katika Kituo cha Kuhifadhia Taarifa (Data Center):** Katika kipindi cha Julai 2025, hadi Machi, 2026 ZICTIA imeendelea kupokea jumla ya mifumo mipya Kumi na mbili (12) na kuihifadhi katika Kituo cha Kuhifadhia Taarifa (Data Centre) kutoka katika taasisi zifuatazo; Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA), Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Rasilimali za Baharini Zanzibar (ZAFIRI), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Kamisheni ya Wakfu na Mali Amana, Mahkama Kuu, Kamisheni ya Ardhi (COLA), Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC), Wizara ya Vijana, Wanawake na Watoto, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (ZPPRA) na Baraza la Taifa la Wafanyabiashara Zanzibar.

e. **Kuwapatia mafunzo watendaji wa ZICTIA:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, ZICTIA imewajengea

uwezo wafanyakazi wake kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya muda mfupi, ambapo jumla ya watumishi 18 walishiriki katika makongamano, warsha na mafunzo ya kitaaluma ndani ya nchi ili kuongeza ufanisi kazini. Mafunzo hayo yalihusisha maeneo kama kumbukumbu na nyaraka, ukaguzi, ununuzi na ugavi, masoko, usalama, GIS, uhasibu wa kompyuta na mawasiliano kwa umma. Aidha, wajumbe wa Bodi walipatiwa mafunzo ya tathmini ya utendaji wa vikao, huku wafanyakazi wote wakipatiwa mafunzo ya Muundo wa Utumishi, usalama wa mtandao, pamoja na elimu ya afya na matumizi salama ya TEHAMA.

**Miradi iliyotekelezwa na Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2025 – 2026**

23. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara kupitia Shirika la Mawasiliano Zanzibar inatekeleza miradi ifuatayo:

    a. **Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Taarifa Fumba Awamu ya kwanza.**
    ZICTIA imeendelea na taratibu za manunuzi kwa kuandaa nyaraka sahihi kwa ajili ya kumtafuta mkandarasi kwa lengo la utekelezaji wa mradi huu. Aidha, utengenezaji wa nyaraka za hadidu rejea (TOR) zimekamilika na kukidhi viwango vya Kimataifa kwa kuzingatia taratibu zote ili kumpata mzabuni sahihi, mwenye uzoefu wa kutekeleza mradi (Data Center). Vilevile taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi kwa kazi husika zinaendelea, ambapo kwa upande wa mshauri elekezi ZICTIA inatarajia kupokea fedha kutoka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la upatikanaji wa mshauri elekezi kwa kusimamia na kushauri mradi huu.

b. **Kulaza Mkonga wa Kimataifa wa Baharini Zanzibar (International Gateway)**

ZICTIA imeendelea na utekelezaji wa mradi husika kwa kuanza na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi na Mshauri Elekezi. Aidha, nyaraka za Hadidu Rejea (TOR) tayari zimeshapitiwa na kupitishwa na Bodi ya Zabuni ya ZICTIA kwa hatua zinazofuata. Mradi huu unatarajiwa kutumia jumla ya TZS Bilioni 155.8 hadi kukamilika, ambapo kutokana na changamoto ya upatikanaji wa kiwango hicho cha fedha, ZICTIA imeendelea na kazi ya kutafuta mshirika atakaeweza kuwekeza fedha kwa kufanikisha mradi mzima kwa muda mfupi ikiwa ni mazingatio ya maelekezo ya Serikali. Hivyo, ZICTIA imetiliana saini na Kampuni ya Muungano Cable Limited, inayolenga kufanya upembuzi yakinifu wa kina (Detail Feasibility Study) ya mradi husika.

c. **Uimarishaji wa Mfumo wa Mawasiliano**

Kazi ya kuhamisha Mkonga ili kupisha Miradi ya Maendeleo hususan Miradi ya ujenzi wa barabara imefanyika. Matengenezo hayo yameendelea na kufikia kilimita 50.3 katika maeneo (route) mbali mbali nchini. Maeneo ya Michamvi, Matemwe na Kijundu, hitilafu imetokana na uwekaji wa miundombinu ya maji. Aidha matengenezo yaliyofanyika katika maeneo ya Amani - Kwerekwe, Magogoni, Bumbwini - Mfenesini, Barabara ya Mkapa, Maruhubi, Tunguu - Muyuni - Makunduchi na Pangatupu hadi Mahonda kwa kuhamisha Mkonga ili kupisha ujenzi wa barabara unaoendelea nchini.

d. **Utowaji wa Huduma ya Mtandao katika Maeneo ya Umma (Public WiFi).**

Shirika linaendelea na taratibu za awali za manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kukamilisha kazi ya uwekaji wa huduma ya mtandao katika uwanja wa New Amani Complex na kuendelea na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya watu ikiwemo, Uwanja mpya wa

mpira Fumba, masoko makubwa (Kwerekwe, Mombasa, Darajani, Jumbi na Chuini), Forodhani pamoja na vituo vya mabasi ikiwemo Kijangwani.

e. **Uimarishaji wa Vifaa vya Mkonga wa Mawasiliano.**
ZICTIA imeendelea na kazi ya uimarishaji wa vifaa vya Mkonga kama vile Optical Transport Network (OTN), Router, Switches, Optical Line Terminal (OLT) na CCTV Camera. Utekelezaji wa kazi hii unajumuisha uondoshaji wa vifaa vya zamani na kuweka vifaa vipya vya kisasa pamoja na kuboresha miundombinu. Aidha, utekelezaji wa mradi huu utasaidia katika kuhakikisha vifaa hivyo vinakuwa na uwezo wa kusafirisha kiwango kikubwa cha mawasiliano kinachokidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa kulingana na kasi ya ukuaji wa matumizi ya Mtandao nchini. Shirika limeingia mkataba na kampuni ya ZTE kupitia Wakala wake kwa ajili ya utekelezaji wa kazi husika. Utekelezaji wa mradi huu umeshaanza na tayari msambazaji ameshalipwa Malipo ya awali ya mkataba (Advance Payment) sawa na asilimia 25 ya bei ya mkataba.

f. **Utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar na Upembuzi Yakinifu wa Kituo Mbadala cha kuhifadhia Taarifa - Pemba.**
ZICTIA kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi imeendelea na utekelezaji wa Mradi huu kwa kukamilisha hatua mbali mbali ikiwemo vikao vya wadau (MNO, Government Stakeholders), kuwasilisha Ripoti ya awali "inception report" na kuwasilisha kwa rasimu za Mpango Mkuu wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar na Upembuzi Yakinifu wa Kituo Mbadala cha kuhifadhia taarifa – Pemba.

**Mapato na Matumizi**
***Mapato***

**24. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Shirika la Mawasiliano Zanzibar lilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 16,091,598,760** na kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, ZICTIA imekadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 11,852,446,070** kupitia vyanzo vyake vya mapato, ambavyo ni Matumizi ya Mkonga (Capacity Lease), Huduma ya Mtandao (Internet), Matumizi ya Kituo cha kuhifadhia Taarifa (Data Center) na Tozo za Minara (Tower Levy). Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **Shilingi 9,445,393,318** zimekusanywa sawa na asilimia **79.7** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **58.7** ya makadirio ya mwaka.

**Matumizi**

**25. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika la Mawasiliano Zanzibar lilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 12,559,155,870** kati ya hizo, **Shilingi 2,193,397,200** ni mshahara, **Shilingi 5,365,758,670** ni kazi za kawaida na **Shilingi 5,000,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Shirika lilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 10,496,936,570** kati ya fedha hizo **Shilingi 1,645,047,900** ni mshahara, **Shilingi 4,851,888,670** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 4,000,000,000** kwa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **Shilingi 10,155,087,707.157** zimetumika sawa na asilimia **96.7** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **80.8** ya makadirio ya mwaka.

**Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ)**

**26. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 1 ya mwaka

2024, ikiwa na jukumu la kupanga, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa huduma zote za Serikali Mtandao. Mamlaka hii ni kiungo muhimu katika mabadiliko ya Serikali kuelekea Zanzibar ya kidijitali, ikiwa na dhamira ya kutoa huduma bora, salama na za kuaminika za TEHAMA katika Taasisi za Umma.

27. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na utaratibu wa Serikali wa kutekeleza majukumu yake kwa kutumia Bajeti inayotumia Programu (Program Based Budget PBB), Mamlaka ya Serikali Mtandao inatekeleza Programu Kuu mbili; Huduma za Serikali Mtandao na Uendeshaji Serikali Mtandao na Programu Ndogo Nne ambazo ni Miundombinu na Mifumo ya TEHAMA, Huduma za TEHAMA, Uendeshaji, Utumishi na Mipango pamoja na Uratibu wa Serikali Mtandao Pemba.

28. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mamlaka ya Serikali Mtandao imepanga kutekeleza Majukumu yake kupitia Kazi zifuatazo:

a. Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao katika utumiaji wa mifumo ya TEHAMA;
b. Kuimarisha Mifumo ya pamoja (shared System) ya Serikali Mtandao;
c. Kuimarisha usalama wa mifumo pamoja na kuandaa miongozo mbalimbali ya TEHAMA;
d. Kusimamia mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki;
e. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao pamoja na vituo vya kuhifadhia taarifa vya dharura;
f. Kuanza kutumika kwa mfumo wa Jukwaa la Huduma za Serikali (Unified Digital Government Platform); na
g. Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Mamlaka.

**Utekelezaji wa Programu za Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

***Programu Kuu ya Huduma za Serikali Mtandao***

**29. Mheshimiwa Spika,** Program Kuu ya Huduma za Serikali Mtandao, ina Programu Ndogo mbili ambazo ni Programu Ndogo ya Miundombinu na Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Programu Ndogo ya Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

***Programu Ndogo ya Miundombinu na Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano***

**30. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Programu Ndogo ya Miundombinu na Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:

a. Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) katika juhudi za kuhakikisha ulinzi wa tovuti dhidi ya hatari za mtandaoni kama udukuzi, wizi wa taarifa au mashambulizi ya kimtandao, ilifanya tathmini ya usalama (Security Assessment) ya tovuti za Serikali, ambapo jumla ya tovuti sita (6) za taasisi za umma zilifanyiwa tathmini hiyo. Taasisi hizo ni Ikulu Zanzibar, Tume ya Mipango Zanzibar, ZAECA, Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu, eGAZ pamoja na Mfumo wa ZanMalipo.

b. Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao ni Kufanya tathmini ya mifumo inayoanzishwa katika Taasisi za Umma kabla ya kuanza Matumizi ili kuweza kuhakikisha ubora na utendaji wa mifumo hiyo kwa kuzingatia viwango na miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao. Jumla ya Mifumo Mitano (5) imefanyiwa Tathmini kutoka katika Taasisi ya Usafiri Baharini (Mfumo wa Utoaji Cheti cha Afya na Kadi za

Mabaharia – eSID), Mfumo wa Maafa (Zanzibar Disaster Management Information System - ZDMIS), mfumo wa kitaifa wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni (National Online Business System - NOBS) na Mahkama Kuu Zanzibar (Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mashauri – eCMS). Taarifa ya tathmini imeshawasilishwa katika Tasisi hizo kwa kufanya marekebisho baadhi ya mapungufu yaliyogundulika katika tathmini hiyo.

c. Mamlaka kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeendesha mafunzo maalum ya kugundua na kujilinda na vitishio vya kiusalama (Offensive Security & Defensive Security) katika mifumo na miuondombinu ya TEHAMA, kwa watendaji wa TEHAMA 47 kutoka Taasisi za Serikali ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na vitisho vya kimtandao pamoja na kuimarisha ulinzi wa miundombinu na mifumo ya TEHAMA.

d. Kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (DTP) unaotekelezwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka ya Serikali Mtandao imeanzisha Mfumo maalum wa ZanXchange kwa ajili ya kubadilishana taarifa baina ya Taasisi za Serikali na Taasisi Binafsi kwa kuleta usalama wa mifumo, upatikanaji wa huduma kwa uharaka na urahisi. Kwa sasa Mamlaka inaendelea na zoezi la kuingiza taarifa za taasisi katika mfumo huo.

e. Mamlaka imeweza kutengeneza mfumo wa kusimamia tovuti (Content Management System – CMS) kwa lengo la kurahisisha usimamizi wa maudhui (content) katika tovuti kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huu wa CMS umeundwa ili kuwawezesha watumiaji wenye majukumu tofauti kuingiza, kurekebisha na kufuta maudhui ya tovuti kama vile taarifa za matangazo, habari, nyaraka na picha bila kuhitaji ujuzi wa kina wa lugha za program (Programming Language) kwa mtumiaji wa kawaida.

f. Mamlaka inasimamia Mfumo wa Bajeti na Matumizi Serikalini (BAMAS) mfumo ambao unalengo la kurahisha uandaaji na matumizi ya bajeti kwa kutumia mifumo. Mamlaka imeunganisha Mfumo wa BAMAS na Mfumo wa HR-PayMIS ili kuwezesha mishahara ya watumishi wa Umma kulipwa kwa wakati na kwa ufanisi. Aidha Mfumo wa BAMAS umeunganishwa na mfumo wa Malipo wa mafao kwa wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ZSSF (FUMIS & Employers Portal) kwa lengo la kuhakikisha makato ya Waajiriwa yanalipwa kwa wakati.
g. Mamlaka, katika juhudi za kurahisisha na kuendeleza matumizi ya TEHAMA, inaendelea na utengenezaji wa mfumo wa usajili na malipo kwa wazee wote wenye umri kuanzia wa miaka 70 (Pencheni Jamii). Mfumo huu umekamilika na ulizinduliwa rasmi na Muheshimwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, tarehe 06/05/2026.
h. Mamlaka imetoa ushauri wa kitaalamu pamoja na msaada wa kiufundi kwa Taasisi za Umma katika usimamizi wa mifumo na Miundombinu ya TEHAMA ili kuhakikisha huduma za serikali Mtandano zinapatikana kwa Masaa 24 kwa wananchi wanaotaka huduma za Serikali. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya Taasisi sitini na tisa (69) zilipatiwa msaada wa kitaalmu.

***Programu Ndogo ya Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano***

**31. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Programu Ndogo ya Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:

a. Mamlaka ya Serikali Mtandao imetekeleza jukumu lake la Msingi la Kutoa ushauri wa kitalaam kwa ununuzi wa vifaa vya TEHAMA katika Taasisi za Umma, ambapo jumla ya Taasisi 13 zimepatiwa ushauri ambao ulilenga kuhakikisha

miongozo ya Ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA inafuatwa na kuthibitisha ubora wa vifaa hivyo. Taasisi hizo ni; Baraza la Jiji Zanzibar, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Tume ya Maadili wa Viongozi wa Umma Zanzibar, Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF), Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (OCAGZ) Baraza la Manispaa Magharibi A, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI), Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo na Wizara ya Fedha na Mipango.

b. Mamlaka imeendelea na Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA, kupitia mawazo ya miradi (Concept Note). Jumla ya maombi sita (6) kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA), Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (Human Resource Assessment MIS), Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (Digital Disbursement Solution - DiDiS), Tume ya Utangazaji Zanzibar (Billing System), Tume ya Mipango Zanzibar (Zanzibar Integrated Micro Economic Data Portal - ZAMeDAP), Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Zanzibar Audit Data Management System - ZADMS) yamefanyiwa kazi. Lengo la kupitia mawazo hayo ni kuhakikisha kua pendekezo la mradi wa kutengeneza mfumo linaendana na moingozo na viwango vya TEHAMA vya Serikali.

c. Katika kutekeleza jukumu lake kuu la kuandaa na kusimamia sera, kanuni na miongozo inayohusu maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, Mamlaka ya Serikali Mtandao ilifanya Mapitio na maboresho ya miongozo mitano ya TEHAMA inayotumika Serikalini. Miongozo iliyofanyiwa mapitio ni:

**Government Hardware and Software Specifications:** Muongozo huu unahusiana na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA katika Taasisi za Umma, maboresho yaliyofanyika katika muongozo huu yalilenga kuweka vigezo vipya vya vifaa vya TEHAMA kutokana na kupitwa kwa muda kwa vigezo vilivyopo pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya Teknolojia ibukizi.

**Government ICT Project Review Checklist:** Muongozo huu umefanyiwa Mapitio kutokana na maendeleo na ongezeko la miradi ya TEHAMA Serikalini ili kuleta ufanisi kwa mazingira ya sasa. Mapitio yalilenga kuainisha maeneo yaliyopitwa na wakati, mapungufu yaliyopo pamoja na vipengele vilivyohitaji kuboreshwa ili dodoso liweze kukidhi vigezo vya nyenzo ya tathmini ya miradi ya TEHAMA kabla ya kuidhinishwa na wakati wa utekelezaji. Kupitia mapitio hayo, vipengele mbalimbali vya checklist vilifanyiwa maboresho kwa kuzingatia ulinganifu wa miradi ya TEHAMA na Mipango na Sera za Serikali, mahitaji ya kiufundi, usalama wa mifumo, uendelevu wa miradi pamoja na usimamizi wa gharama.

**Mahitaji ya Mfumo wa Baraza Mtandao (e-Cabinet):** Kuaandaa mahitaji ya mfumo wa Baraza Mtandao utakaotumika kwa Vikao vya Kamati ya Makatibu Wakuu na Vikao vya Baraza la Mapinduzi.

**Uandaaji wa Mfumo wa Pensheni Jamii:** Mfumo umeshakamilika na unatarajiwa kutumika katika malipo ya wazee.

**Biofin Mfumo wa Vivutio vya Utalii:** Mfumo umeshakamilika na unatarajiwa kutumiwa katika utoaji wa huduma katika vivutio vya utalii.

d. Kuandaa Muongozo wa Akili Unde katika Utumishi wa Umma Kutokana na kasi ya maendeleo ya teknolojia za kidijitali duniani, hususan kuongezeka kwa matumizi ya Akili Unde (AI) katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii, Mamlaka ya Serikali Mtandao imechukua hatua

madhubuti ya kuandaa Muongozo wa Matumizi ya Akili Unde (AI) katika Utumishi wa Umma. Muongozo huu unalenga kuweka misingi na miongozo ya kitaalamu itakayosaidia Taasisi za Umma katika kubuni, kuendeleza na kutumia mifumo ya kidijitali inayotumia Akili Unde, kwa kuzingatia viwango vya ufanisi, usalama wa taarifa, uwazi pamoja na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

e. Mamlaka imeendelea kutekeleza jukumu lake la usimamizi na uratibu wa masuala ya TEHAMA kwa kushiriki kikamilifu katika mapitio ya Mkakati wa Akili Unde (AI) wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushiriki huo umeiwezesha Zanzibar kuzingatia na kuendana na mwelekeo wa kikanda katika matumizi ya teknolojia za kisasa, sambamba na kunufaika na fursa zinazotokana na ushirikiano wa Kikanda.

f. Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi ya Zanzibar ya Wahasibu, Wakaguzi wa Hesabu na Washauri wa Kodi *(Zanzibar Insitute of Accountatnt, Auditors and Tax Consultant - ZIAAT)* ilifanya mapitio ya Sera ya TEHAMA ya Taasisi hiyo kwa lengo la kuhakikisha kuwa Sera hio inaendana na Sera na Miongozo ya TEHAMA Serikalini, kiujumla Sera hiyo imekidhi viwango na miongozo iliyopo.

g. Mamlaka imeendela kuzingunisha Taasisi za Serikali na Mfumo wa **ERMS (Enterprise Resourse Management Suit).** Mfumo huu unatumika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ambapo husimamia shughuli za ndani za Taasisi, kuboresha utendaji kazi, kusimamia matumizi mazuri ya rasilimali na kuweza kubadilishana taarifa miongoni mwa Idara/Vitengo ndani ya Taasisi husika pamoja na kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji. Jumla ya Taasisi tatu zimeunganishwa na mfumo huo ambazo ni; Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC), Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) na Viwanda vya Idara Maalum

za SMZ pamoja na kupatiwa uelewa kwa watendaji wake 67 kwa matumizi ya mfumo huo.

h. Mamlaka imeendelea kutoa mafunzo ya Ofisi Mtandao kwa Taasisi za Umma kwa lengo la kuhakikisha kua Taasisi za Serikali zinatunza kumbukumbu kwa njia ya Mifumo na kuitumia katika shughuli za kila siku za Taasisi. Jumla ya wafanyakazi arobaini na tano (45) wamepatiwa mafunzo kutoka katika taasisi zifuatazo:- Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana Na Madawa ya Kulevya Zanzibar, Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar, Tume ya Ushindani Halali wa Biashara Zanzibar (ZFCC), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Chuo Cha Mafunzo Zanzibar na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

***Programu Kuu ya Uendeshaji wa Serikali Mtandao***

**32. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu mbili ndogo ambazo ni Programu Ndogo ya Uendeshaji, Utumishi na Mipango na Programu Ndogo ya Uratibu wa Serikali Mtandao Pemba.

***Programu Ndogo ya Uendeshaji, Utumishi na Mipango***

**33. Mheshimiwa Spika,** Kupitia Programu Ndogo ya Uendeshaji, Utumishi na Mipango, Mamlaka imeweza kutekeleza yafuatayo:

a. Katika kuimarisha ufanisi na tija kwa wafanyakazi Ofisi imefanikiwa kulipa posho la likizo za wafanyakazi saba (7). Aidha, imeendelea kuwajengea uwezo Watendaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu, jumla ya Maafisa 16 wa kada ya TEHAMA wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi

yanayohusiana na Usimamizia wa miradi ya TEHAMA na njia bora za ufuatiliaji na uimarishaji wa mifumo ya TEHAMA. Vile vile watumishi tisa (9) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi.

b. Mamlaka ya Serikali Mtandao imetiliana saini Hati za Makubaliano (MoU) mbili baina ya Ofisi na Stanbic Bank Tanzania Limited na Wakala wa Usajili wa Mtukio ya Kijamii Zanzibar kwa lengo la kurahisisha na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa njia ya kidijitali.

c. Mamlaka imefanya marekebisho madogo ya Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao namba 1 ya mwaka 2024, kufuatia agizo la Wizara ya Mawasiliano Teknolojia ya Habari na Ubunifu, katika kifungu cha 8 kinachohusiana na Uanzishaji na Muundo wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtando na kifungu cha 38 kinachoelezea kuanzishwa kwa Kituo cha Opresheni ya Usalama cha Serikali Mtandao na taratibu za mabadiliko haya zinaendelea.

d. Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) imeshiriki kikamilifu katika Maonesho ya 12 ya Kimataifa ya Biashara – Dimani yaliyofanyika katika Viwanja vya Nyamanzi, Zanzibar, kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi na wadau mbalimbali kuhusu umuhimu na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji na upatikanaji wa huduma za Serikali. Jumla ya wananchi **320** walitembelea katika banda la Mamlaka ya Serikali Mtandao.

e. Mamlaka ya Serikali Mtandao imeendelea na programu ya kutoa elimu kwa umma kwa kupitia redio, Televisheni, mitandao ya kijamii na vipeperushi. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Mamlaka imerusha hewani vipindi vinne vya Television na Vipindi vinne vya Radio vyenye maudhui ya mageuzi ya Kidijitali katika utoaji wa huduma za Seikali. Aidha taasisi imeandaa Makala ya hali halisi juu ya mapinduzi makubwa ya TEHAMA yanayofanyika Zanzibar ikiwa ni sehemu ya shamrashamra

za Maadhimisho ya Sherehe za miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyochapishwa katika Gazeti la Zanzibar Leo na kurushwa hewani katika Shirika la Utangazaji Zanzibar.

f. Mamlaka imeshiriki katika kikao cha kimkakati cha ubunifu na fursa za ushirikiano (Innovation and Business Matchmaking Session) kilichoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kupitia kitengo cha Accelerator Labs. Kikao hicho kilifanyika katika Ofisi za Umoja wa Mataifa Zanzibar na kimewakutanisha wadau mbalimbali pamoja na ujumbe wa makampuni kutoka Japani ikiwemo Toppan Ecquaria, Hakki Africa, Synspective na Pegara Japan kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika nyanja za ubunifu wa kidijitali, huduma jumuishi za kifedha pamoja na uwekezaji. Kupitia ushiriki huo, eGAZ imepata fursa ya kuonesha jitihada zake katika mifumo ya TEHAMA pamoja na kujadili maeneo ya ushirikiano wa muda mrefu ili kuchochea mapinduzi ya kidijitali na ukuaji wa uchumi na utalii endelevu Zanzibar.

g. Mamalaka imefanikiwa kutekeleza jukumu lake la kutoa elimu kwa wadau wa TEHAMA wa elimu ya juu ambapo kwa kipindi cha Januari 2025 hadi Machi 2026 imetoa elimu kwa wanafunzi wa **Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) – Tunguu** kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu matumizi ya **e-Governance**. Muhadhara huo umehudhuriwa na zaidi ya wanafunzi 150 pamoja na wahadhiri. Mada zilizo wasilishwa ni pamoja na uendeshaji wa mifumo ya Serikali Mtandao na namna teknolojia inavyorahisisha upatikanaji wa huduma za Serikali na Umuhimu na madhara ya Matumizi ya Akili Unde kwa wanafunzi wa vyuo.

h. Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) imeshiriki katika Kikao Kazi cha 6 cha Serikali Mtandao kilichoandaliwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao Tanzania (eGA) katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC). Kikao hicho kimewakutanisha Viongozi waandamizi, wataalamu wa TEHAMA pamoja na wadau wa maendeleo

kutoka Taasisi mbalimbali za umma kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya pande mbili za Muungano katika maendeleo ya mifumo ya kidijitali. Kupitia kikao hicho, washiriki wamebadilishana uzoefu kuhusu sera za TEHAMA, usimamizi wa mifumo ya kidijitali, pamoja na mbinu bora za kukuza uchumi wa kidijitali kupitia mifumo Jumuishi.

i. Mamlaka imeshiriki katika Mkutano wa Pili wa Kimataifa wa *Digital Workplace Summit Zanzibar (IDWS – 2026)* uliofanyika katika Hoteli ya Golden Tulip Airport Zanzibar. Mkutano huo umewakutanisha zaidi ya washiriki 300 kutoka Nchi mbalimbali wakiwemo wataalamu wa teknolojia, Viongozi wa Taasisi na wadau wa Sekta ya TEHAMA. Katika mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Dkt. Said Seif Said amewasilisha wasilisho lenye mada ya *"Zanzibar: The Transformative Power of AI and Technologies in the Workplace – Utilize Emerging Technologies such as AI, Block chain and IoT Empowering People for the Digital Era."* Kwa Washiriki. Ushiriki huo umeongeza uelewa kuhusu nafasi ya Zanzibar katika mageuzi ya kidijitali hasa katika sekta za umma, kuimarisha ushirikiano na wadau wa Kimataifa pamoja na kufungua fursa za matumizi ya teknolojia zinazoibuka katika kuboresha mazingira ya kazi na utoaji wa huduma za umma.

j. Mamlaka ya Serikali Mtandao imefanya kikao kazi pamoja na kuwapatia Mafunzo Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA ya Baraza la Wawakilishi. Kikao hicho kililenga kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati hio pamoja na kuwa na uelewa wa majukumu ya eGAZ na kuwasilisha changamoto zinazoikabili Mamlaka kwa lengo la kupata usimamizi na kuweza kufikishwa sehemu husika na Wajumbe wa Kamati hio.

### *Muhtasari wa Taarifa ya Upatikanaji wa Fedha*

**34. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mamlaka ya Serikali Mtandao imeidhinishiwa jumla ya

**Shilingi 4,620,500,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,801,200,000** ni ruzuku kwa ajili ya matumizi Mengineyo **na Shilingi 1,819,300,000** kwa ajili ya Ruzuku ya Mshahara.

35. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka ya Serikali Mtandao ilikadiria kutumia jumla ya **Shilingi 3,155,491,179.** Kati ya hizo, **Shilingi 1,147,350,849** zilipangwa kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 2,008,140,330** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya fedha zilizopatikana ni **Shilingi 2,285,095,537** sawa na asilimia **72** ya makadirio. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,111,562,868** ni za mshahara sawa na asilimia **97** ya kiasi cha fedha za mshahara kilichopangwa. **Shilingi 1,173,532,669** za kazi za kawaida sawa na asilimia **58** ya fedha zilizopangwa. Kama inavyoonekana katika **Kiambatisho nambari 1B**

***Programu Ndogo ya Uratibu wa Serikali Mtandao Pemba.***

36. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Ofisi ya Uratibu Mamlaka ya Serikali Mtandao Pemba na ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma bora kwa urahisi katika Taasisi za Umma kisiwani Pemba. Kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Serikali Mtandao Pemba, Mamlaka imeweza kutekeleza yafuatayo:

    a. Mamlaka imefanya mafunzo ya mfumo wa Barua Pepe wa Serikali (GMS), Ofisi Mtandao (e-Office) na mfumo wa Saini ya Kidijitali (Digital Signature) kwa Maafisa TEHAMA na Maafisa kumbukumbu Serikalini ambapo jumla ya Maafisa **148** walishiriki katika mafunzo hayo. Mafunzo hayo yalilenga kuboresha utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya Teknologia ya Habari na Mawasiliano ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Hii ni kutokana na ukaguzi uliofanywa na Mamlaka kwa baadhi ya Taasisi za Umma na kubaini changamoto nyingi zinazowakabili watumiaji

wa mifumo hiyo ikiwemo uelewa mdogo katika matumizi ya mifumo.

b. Mamlaka imetoa mafunzo ya ndani kwa watendaji wake 16 mafunzo hayo yalililenga kutoa elimu juu ya namna ya kujikinga na majanga ya moto yanayoweza kutokezea katika maeneo yao ya kazi. Mafunzo hayo yametolewa na Maafisa kutoka Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar.

c. Mamlaka inaendelea kuzipatia Tasisi huduma ya *Virtual Private Network (VPN)* ili kuwezesha Taasisi hizo kuunganishwa na mkonga wa Serikali na kuweza kutumia Mifumo kutokana na kuwa kuna baadhi ya Taasisi za umma hazijafikiwa na miundombinu hiyo. Taasisi zilizopatiwa huduma hiyo ni Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Micheweni, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

d. Mamlaka inaendelea kutatuwa changamoto za kitaalamu zinazojitokeza katika mifumo ya TEHAMA ya Serikali ikiwa ni utekelezaji wa majukumu yake ya kusimamia mifumo hiyo katika Taasisi za Umma jumla ya Taasisi tisa (9) zimepatiwa ushauri wa kitaalamu na kutatuliwa changamoto zao.

e. Mamlaka imewapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wawili yanayohusiana na uandaaji wa mpango mkakati wa maendeleao ya utoaji wa habari kidigitali na Usimamizi wa Mnyororo wa Ununuzi na Ugavi kwa njia ya kidigitali. Wafanyakazi wanne wamepatiwa posho la likizo na mfanyakazi mmoja emepewa posho la ufiwa.

f. Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar imetoa mafunzo kuhusu maboresho ya mfumo wa ZanMalipo (Ankara Jumuishi) ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wateja wanapofanya malipo. Mfumo huo utamuwezesha mwananchi kulipa mara moja wakati anapohitaji huduma ambayo inatozwa kodi na Taasisi zaidi ya moja. Mafunzo hayo yametolewa kwa Wahasibu na Maafisa TEHAMA wote katika Taasisi za Umma 23 zinazohusika na ukusanyaji wa mapato.

g. Mamlaka imetoa mafunzo ya siku moja kuhusu umuhimu wa elimu ya TEHAMA kwa vijana katika kongamano la kuadhimisha kilele cha siku ya vijana duniani lililoandaliwa na Wizara ya Hapari, Vijana, Utamaduni na Michezo lililofanyika katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Wete ambalo lilihudhuriwa na vijana 400. Mafunzo hayo yameonesha fursa zinazopatika katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa vijana ikiwemo upatikanaji wa ajira pamoja na kuchochea ubunifu na ujasiriamali.
h. Wafanyakazi wawili wameshiriki mafunzo ya wiki mbili yanayohusu usimamizi wa mifumo ili kuongeza udhibiti katika mifumo hiyo, mafunzo hayo yamefanyika kwa awamu mbili, awamu ya kwanza Dodoma na awamu ya pili Dar-es-salaam. Mafunzo hayo yana lengo la kuongeza udhibiti katika usimamizi wa mifumo na kuongeza usalama na uwezo katika server ili kutatua changamoto za mifumo zinazojitokeza.

**37.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu wa Serikali Mtandao, Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 cha Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilikadiria kutumia jumla ya **Shilingi 510,423,364**. Kati ya hizo, **Shilingi 297,054,604** zilipangwa kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 213,368,760** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya fedha zilizopatikana ni **Shilingi 413,176,892** sawa na asilimia **81** ya makadirio. Kati ya fedha hizo **Shilingi 304, 353,475** ni za mshahara sawa na asilimia **102** ya kiasi cha fedha za mshahara kilichopangwa. **Shilingi 108,823,41**7 za kazi za kawaida sawa na asilimia **51** ya fedha zilizopangwa. Ongezeko hilo la mshahara linatokana na tafauti ya mshahara kwa watendaji waliohamishiwa eGAZ. Kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 1B.**

## E. MUELEKEO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

***Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA)***

**38. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Shirika la Mawasiliano Zanzibar imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

a. Kulaza Mkonga wa Kimataifa wa Baharini (International Gateway)
b. Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Kuhifadhia Taarifa Fumba (Tier IV Data Center)
c. Ujenzi wa Kituo Mbadala cha Kuhifadhia Taarifa Pemba (Disaster Recovery Center)
d. Utowaji wa Huduma ya Mtandao katika Maeneo ya Umma (Public Wi-Fi)
e. Uanzishwaji wa Mji wa Teknolojia (Technology Park).
f. Kutoa mafunzo ya nje na ndani kwa wafanyakazi wa Shirika.
g. Kufanya matengenezo ya Mkonga katika maeneo yaliyoathirika.
h. Kufikisha Mkonga katika maeneo ya kimkakati kama vile AFCON City, Mangapwani port na Mji wa Serikali Kisakasaka
i. Uimarishaji wa Vifaa vya kituo cha kuhifadhia Taarifa (Data Cnter)
j. Uondoshaji wa Mkonga ili kupisha ujenzi wa barabara unaondelea nchini

**39. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mradi wa Mji wa Teknolojia Fedha zinatoka katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, Miradi ya Kulaza Mkonga wa Kimataifa wa Baharini, Ujenzi Kituo cha Kuhifadhia Taarifa, Ujenzi wa Kituo Mbadala cha Kuhifadhia Taarifa na Utoaji wa Mtandao katika Maeneo ya Umma itatekelezwa kwa njia ya Usanifu/

Uhandisi, Ununuzi wa Vifaa na Huduma, Ujenzi na Ufadhili wa Mradi (Engineering, Procurement, Construction and Financing - EPC+F)

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**
***Makadirio ya Makusanyo ya Mapato***

**40. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Shirika la Mawasiliano Zanzibar limekadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 17,000,000,000** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni Matumizi ya Mkonga (Capacity Lease), Huduma ya Mtandao (Internet), Matumizi ya Kituo cha kuhifadhia Taarifa (Data Center) na Tozo za Minara (Tower Levy) **Kiambatisho Namba 7**.

***Makadirio ya Matumizi***

**41. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi, Shirika limepanga kutumia jumla ya **Shilingi 45,703,668,671**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,700,000,000** ni mshahara na **Shilingi 9,638,668,671** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 33,365,000,000** kwa ajili ya kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 31,365,000,000** ni mgao kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na **Shilingi 2,000,000,000** zitatolewa na Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA). **Kiambatisho Namba 8**.

***Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ)***

**42. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Mamlaka ya Serikali Mtandao itakuwa inatekeleza majukumu yake katika Programu kuu moja ambayo ni Uendeshaji wa Mifumo ya Mawasiliano Zanzibar. Programu hii ina programu ndogo moja Mifumo ya Serikali Mtandao, Huduma inayotolewa na Programu hii ni Usimamizi wa mifumo ya Serikali Mtandao.

43. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imetokana na majukumu mahsusi ambayo ni; Kuandaa na kusimamia Sera, Kanuni na Miongozo ya maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma, Kuandaa Mipango ya Kitaifa ya maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma pamoja na kuratibu utekelezaji wa mipango hiyo, Kuishauri Serikali katika matumizi bora ya TEHAMA katika uendeshaji na utoaji huduma za umma; Kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma kwa ajili ya kuimarisha ufanisi na uthabiti wa utendaji kazi wa Serikali, utoaji huduma kwa umma pamoja na kupeyana na kubadilishana taarifa baina ya taasisi za Serikali, baina ya Serikali, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla; Kutoa miongozo na kufanya tathimini ya ubora wa mifumo ya TEHAMA katika Utumishi wa Umma na kuhakikisha kwamba ubora wa vifaa vya TEHAMA katika Utumishi wa Umma vinakuwa katika viwango vinavyokubalika, Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera ya usalama wa TEHAMA na muongozo wa matumizi yake katika Utumishi wa Umma.

44. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027 Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

a. Upanuzi na uboreshaji wa Miundonmbinu ya TEHAMA katika Taasisi za Umma( Gov Net).
b. Usimamizi wa Mifumo ya Kifedha na Ukusanyaji wa Mapato
c. Kuwajengea uwezo watendaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (Profesional Capacity Building)
d. Kuhakikisha mifumo yote ya Serikali inasomana (Enteroperability) na iko salama dhidi ya mashambulizi ya Kimtandao.
e. Kufanya utafiti na ubunifu kwa Teknelojia mpya zinazoibuka.

f. Kuanza kutumika kwa mfumo wa Jukwaa la Huduma za Serikali (Unified Digital Government Platform) na
g. Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Mamlaka.

45. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar ili iweze kutekeleza majukumu yake, kwa mwaka wa fedha 2026/2027, inahitaji jumla ya **Shilingi 15,421,340,000**. Kati ya fedha hiz**o Shilingi 3,457,240,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 1,964,100,000** kwa ajili ya matumizi ya Mishahara na **Shilingi 10,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Maendeleo. Fedha hizo zinatokana na mgao wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## F. MWELEKEO WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

46. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji kwa kila Programu zinazosimamiwa na Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu Pamoja na Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, kwa ruhusa yako sasa, naomba kuwasilisha Mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha **2026/2027.**

47. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa mpango wake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2025-2030; Maelekezo ya Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoyatoa wakati akizindua Baraza la Kumi na Moja la Wawakilishi tarehe 10 Novemba, 2025; Ahadi na Maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa; Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050; Mpango wa Taifa wa Maendeleo Zanzibar – ZADEP (2021 – 2026) na Sera ya Kidijitali ya Zanzibar ya Mwaka 2026. Aidha, Wizara, imezingatia Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

48. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Miongozo hiyo, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu itajikita katika utekelezaji wa vipaumbele vifuatavyo:

a. **Kuweka mazingira wezeshi kwa kutunga, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa miongozo inayosimamia Sekta ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:** kwa kusimamia utekelezaji wa Sera ya Kidijitali ya Zanzibar ya mwaka 2026; kuendelea na hatua za kuandaa Rasimu ya Sheria ya Kampuni Chipukizi na Ubunifu (Startups and Innovation Act); kutunga Sheria ya TEHAMA na kukamilisha hatua za kuandaa Rasimu ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

b. **Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha Anuani ya Makaazi**: kwa kuendelea kutoa, kusajili na kuhakiki Anuani za Makaazi, kuendeleza matumizi ya Mfumo huo katika utoaji wa huduma kidjitali pamoja na kutoa elimu na uelewa wa mfumo.

c. **Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa kampuni chipukizi (Startups):** kwa kuendelea kutoa mafunzo ya TEHAMA na elimu ya dijitali kwa wananchi kupitia Vituo vya TEHAMA jamii pamoja na kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Ubunifu na Ujasiriamali wa TEHAMA Fumba kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali.

d. **Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano nchini kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na Makampuni yanayotoa Huduma za Mawasiliano:** kwa kujenga minara ya mawasiliano katika maeneo yenye changamoto za upatikanaji wa huduma ya mawasiliano Unguja na Pemba.

**Programu zinazosimamiwa na kutekelezwa na Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu kwa mwaka wa fedha 2026/2027.**

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Mawasiliano Teknolojia ya Habari na Ubunifu itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sekta ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu kupitia Programu Kuu tatu (3) ambazo ni: **Programu Kuu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (TEHAMA),** Programu hii ina Program ndogo mbili (Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA na Programu Ndogo ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Ubunifu katika TEHAMA), **Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu,** Progarm hii ina Program Ndogo tatu (Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Tafiti za Wizara na Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba) na **Programu Kuu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Mawasiliano Zanzibar,** Programu hii ina Programu ndogo moja (Programu Ndogo ya Mifumo ya Serikali Mtandao),

50. **Mheshimiwa Spika,** Programu zilizoelezewa katika makadidio ya bajeti hii zimewekewa malengo mahsusi, matokeo ya muda mrefu yatakayopatikana, huduma zitakazotolewa, shabaha na viashiria vitakavyotumika kupima utekelezaji wa huduma zitakazotolewa kupitia Sekta za Wizara hii.

**Muhtasari wa Maelezo kwa Kila Programu na Malengo yanayotarajiwa Kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

***Programu Kuu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (TEHAMA)***

51. **Mheshimiwa Spika,** matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika Programu hii ni kuimarika kwa miundombinu na huduma bora, salama na za uhakika za Teknolojia ya Habari

na Mawasiliano (TEHAMA), pamoja na kuongezeka kwa usalama wa taarifa binafsi na mifumo ya TEHAMA. Aidha, Programu hii itachochea ukuaji wa ubunifu na mageuzi ya kidijitali, na hivyo kuongeza fursa za ajira kupitia sekta ya ubunifu. Programu hii ina Programu Ndogo mbili (2), ambazo ni: Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA na Programu Ndogo ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Ubunifu katika TEHAMA. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 tunaomba Barazalyako liidhinishe jumla **Shilingi 668,283,000** kwa programu hii.

***Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA***

52. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano na Miundombinu na ina lengo la kusimamia uwepo wa miundombinu na huduma bora za TEHAMA zilizo salama na endelevu kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji yanayotokana na uwekaji wa Sera na Sheria Rafiki. Huduma zinazotolewa katika Programu hii ni Usimamizi wa Miundombinu ya TEHAMA na Usimamizi wa Huduma za TEHAMA.

***Idara ya Mawasiliano na Miundombinu***

53. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Idara ya Mawasiliano na Miundombinu kupitia Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA imepanga kusimamia na kutekeleza kazi zifuatazo:

    a. Kuweka mazingira wezeshi kwa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati, Sheria na Miongozo ya Sekta ya Mwasiliano inayotolewa na Mamlaka zinazosimamia Sekta ya Mawasiliano.
    b. Kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha Biashara Mtandao kwa kimarisha Mfumo wa Anuani za Makaazi kwa kuhakiki taarifa za Anuani za Makaazi.

c. Kutoa Elimu na Uelewa wa Utekelezaji wa Mfumo wa Anuani za Makaazi kwa Wataalam wa Serikali za Mitaa wakiwemo Masheha pamoja na watoa huduma za mawasiliano.
d. Kuanzisha na kuweka udhibiti wa Mfumo wa ndani wa Wizara kwa njia ya kielektroniki.
e. Kuweka na kuhifadhi Taarifa za Maafisa TEHAMA kwa njia ya kielektroniki
f. Kuanzisha Mfumo wa usajili na utoaji wa Leseni kwa Wataalam wa Sekta ya Mawasiliano kwa njia ya Kielektroniki.

**54. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA inaombewa kutumia jumla **Shilingi 238,718,000** kwa kazi za kawaida ili kufanikisha shughuli zilizoainishwa.

***Programu Ndogo ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Ubunifu katika TEHAMA.***

**55. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Ubunifu katika TEHAMA inasimamiwa na Idara ya Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Pamoja na Idara ya Ubunifu. Programu hii ina lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa taarifa binafsi pamoja na mifumo ya TEHAMA, na kukuza na kushajihisha ubunifu wa TEHAMA kwa kuweka mazingira wezeshi yanayotokana na uwepo wa sera na sheria rafiki. Huduma zinazotolewa katika Programu hii ni Usimamizi wa Usalama Mtandao na Taarifa Binafsi, Usimamizi na Udhibiti wa Maendeleo ya Ubunifu, Uimarishaji wa Ubunifu na Mageuzi ya Kidijitali, pamoja na Usimamizi na Uanzishaji wa Vituo vya Ubunifu.

***Idara ya Usalama Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi***

**56. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Idara ya Usalama Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi kupitia

Programu Ndogo ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Ubunifu katika TEHAMA imepanga kusimamia na kutekeleza kazi zifuatazo:

a. Kuandaa Sera, Mikakati na miongozo ya Usalama na Ulinzi wa Mtandao na Taarifa Binafsi
b. Kuanzisha na kusimamia Kituo cha Usalama wa miundombinu muhimu ya Taarifa
c. Kufuatilia na kufanya tathmini ya usalama wa mtandao kwa kufanya uchambuzi wa vihatarishi vya usalama mtandaoni
d. Kusimamia, kufuatilia na kufanya udhibiti wa taka za kielektroniki.

**57. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Programu Ndogo ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Ubunifu katika TEHAMA inaombewa kutumia jumla **Shilingi 429,565,000** kwa kazi za kawaida ili kufanikisha shughuli zilizoainishwa.

***Idara ya Ubunifu***

**58. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/20278 Idara ya Ubunifu kupitia Programu Ndogo ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na ubunifu katika TEHAMA imepanga kusimamia na kutekeleza kazi zifuatazo:

a. Kuandaa Sera, Mikakati na Miongozo ya Ubunifu wa Kidijitali
b. Kufanya utafiti na kutathmini mazingira ya Ubnifu na Ujasiriamali wa Kidijitali Zanzibar
c. Kukuza na kuratibu mazingira wezeshi ya Ubunifu wa Kidijitali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi (PPP)
d. Kuratibu, kusimamia na kufanya tathmini ya matumizi ya Teknolojia zinazoibukia
e. Kuratibu na kuwezesha uanzishwaji wa Kampuni Chipukizi (Startups) ikiwemo kuwaunganisha waanzilishi wa Kampuni Chipukizi na fursa zinazopatikana Kitaifa na Kimataifa.

***Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara.***

**59.** **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya Programu hii ni kuwepo kwa uratibu wa Shughuli za Wizara katika Sera, Mipango ya Kisekta Pamoja na usimamizi wa Rasilimali Watu. Program hii ina Programu Ndogo tatu (3) ambazo ni: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Program Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti Za Wizara na Program Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

**60.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Programu Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu inaombewa kutumia jumla **Shilingi 47,302,177,000** kwa kazi za kawaida na kazi za Maendeleo ili kufanikisha shughuli zilizoainishwa.

***Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji***

**61.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina lengo la kuimarisha hu duma za ofisi ma usimamizi wa Rasilimali Watu katika Wizara. Huduma zinazotolewa katika Programu hii ni Uimarishaji wa Mazingira ya Kazi Katika Wizara na Usimamizi wa Rasilimali Watu na Huduma katika Wizara.

***Idara ya Uendeshaji na Utumishi***

**62.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia Programu hii imepanga kusimamia na kutekeleza kazi zifuatazo:

a. Kusimamia masuala ya kiutumishi na uendeshaji wa Wizara kwa kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi na kuwapatia vitendea kazi pamoja na kuvifanyia matengenezo ili kuongeza ufanisi wa kazi na kuratibu vikao vya Kamati za Uongozi na Tendaji.

b. Kutoa Makala na Machapisho kuhusu utekelezaji wa shughuli na mafanikio ya Wizara pamoja na kuratibu safari za kikazi za ndani na nje ya nchi kwa wafanyakazi.
c. Kuwajengea uwezo watendaji ili kuongeza ujuzi, ufanisi na tija kwa wafanyakazi wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa mujibu wa Mpango wa Mafunzo wa Wizara.
d. Kufanya matengenezo ya Vifaa, vyombo vya moto na ofisi ili kuweka mazingira mazuri ya kutendea kazi.

**63. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Programu Ndogo ya Usamamizi wa Utawala na Uendeshaji inaombewa kutumia jumla ya **Shilingi 4,365,222,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,447,600,000** ni mshahara na Shilingi **1,917,622,000** ni matumizi mengineyo.

***Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara***

**64. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ina lengo la kuhakikisha Mipango na Sera katika Sekta ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu zinatayarishwa Pamoja na kufuatilia utekelezaji wake. Huduma zinazotolewa katika Programu hii ni Uibuaji na Usimamizi wa Sera za Wizara, Uibuaji wa Tafiti na Usimamizi wa Takwimu za Wizara, Utayarishaji na Usimamizi wa Mipango na Bajeti na Ufuatiliaji na Tathmini ya Kazi za Wizara.

***Idara ya Mipango Sera na Utafiti***

**65. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara imepanga kusimamia na kutekeleza kazi zifuatazo:

a. Kuandaa bajeti ya Wizara pamoja na kutoa mafunzo ya utayarishaji wa bajeti kwa watendaji wa Wizara kulingana na Miongozo inayotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango
b. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Wizara ikiwemo Miradi ya Maendeleo pamoja na kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na bajeti.
c. Kuratibu uandaaji na mapitio ya Sera, Sheria, Mikakati, na Miongozo ya Sekta zinazosimamiwa na Wizara
d. Kukusanya na kuchambua takwimu za maendeleo ya Sekta na kuweka Mpango bora wa utunzaji kumbukumbu za takwimu kwa kuandaa mfumo wa kielektroniki wa uhifadhi wa takwimu
e. Kuandaa Muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Utekelezaji wa Kazi za Wizara
f. Kuratibu na kuandaa vikao vya mashirikiano baina ya Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**66. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara inaombewa kutumia jumla ya **Shilingi 41,478,595,000** kwa kazi za kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo **Shilingi 113,595,000** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 41,365,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo Shirika la Mawasiliano ZICTIA na Mamlaka ya Serikali Mtandao eGAZ.

***Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba***

**67. Mheshimiwa Spika**, Programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba na ina lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa ipasavyo kwa upande wa Pemba. Huduma inayotolewa katika Programu hii ni Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba.

***Ofisi Kuu Pemba***

**68. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Ofisi Kuu Pemba kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba imepanga kusimamia na kutekeleza kazi zifuatazo:

a. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa watendaji ikiwemo kusimamia upatikanaji wa huduma muhimu za uendeshaji wa Ofisi, kufanya matengenezo ya Jengo la Ofisi, ununuzi wa Vifaa vya kufanyia kazi pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao.
b. Kuwajengea uwezo watendaji kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ili waweze kufanya kazi zao kwa weledi na ufanisi.
c. Kutoa elimu ya TEHAMA kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii kwa wananchi
d. Kuratibu na kuendeleza matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makaazi.

**69. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa fedha 2026/2027, Programu hii Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inaombewa kutumia jumla ya **Shilingi 1,458,360,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo, **Shilingi 611,860,000** ni mshahara na **Shilingi 846,500,000** ni matumizi mengineyo.

***Programu Kuu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Mawasiliano Zanzibar***

**70. Mheshimiwa Spika,** matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika Programu hii ni kuimarika kwa mifumo ya mawasiliano na huduma za kidijitali zinazotolewa na Serikali, ili ziwe jumuishi, salama, zenye ufanisi na zinazopatikana kwa urahisi kwa wananchi na wadau wote. Aidha, Programu hii itachangia kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa mifumo ya kidijitali ya Serikali, pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa ajili ya maamuzi ya maendeleo ya

Taifa. Programu hii ina ***Programu Ndogo moja, ambayo ni Programu Ndogo ya Mifumo ya Serikali Mtandao.***

71. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Programu hii inaombewa kutumia jumla **Shilingi 5,421,340,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 3,457,240,000** kwa kazi za kawaida na **Shillingi 1,964,100,000** za Mshahara.

72. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar. Programu hii inalenga kuongeza matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma za umma, kuboresha uwazi, uwajibikaji na kasi ya utoaji huduma kupitia mifumo ya Serikali Mtandao. Huduma zinazotolewa katika Programu hii ni Usimamizi wa Mifumo ya Serikali Mtandao.

## MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI NA UBUNIFU KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

73. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu ili kuweza kutekeleza majukumu na malengo yake yaliyoainishwa katika Programu Kuu tatu (3) katika hotuba hii. Naomba kutoa Hoja kwamba Baraza lako liidhinishe jumla ya **Shilingi 53,391,800,000** kwa ajili ya matumizi ya Kazi za Kawaida na Kazi za Maendeleo.

### *Matumizi ya Kazi za Kawaida*

74. **Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha hizo **Shilingi 12,026,800,000** ni kwa ajili ya matumizi ya Kazi za Kawaida na Mshahara. Ufafanuzi wa Matumizi yake ni:
    a. **Shilingi 3,059,460,000** ni matumizi ya Mshahara (PE)
    b. **Shilingi 3,546,000,000** ni matumizi Mengineyo (OC)

c. **Shilingi 1,964,100,000** ni Ruzuku ya Mshahara (Subvention Salary)
d. **Shilingi 3,457,240,000** ni Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (Subvention OC)

***Matumizi ya Miradi ya Maendeleo***

**75. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 41,365,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za maendeleo, ambapo fedha zote zinatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Shirika la Mawasiliano ZICTIA na Mamlaka ya Serikali Mtandao eGAZ.

## SHUKURANI NA HITIMISHO

***Shukurani***

**76. Mheshimiwa Spika,** kabla sijamaliza hotuba hii naomba nitumie fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na ustahamilivu wakati wote nilipokua nikitoa maelezo ya Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na ubunifu. Ni imani yangu kwamba Baraza lako Tukufu litatoa michango ambayo itasaidia Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo ya kuwahudumia wananchi wetu na hatimae kuipitisha Bajeti hii kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Wizara zilizopangwa kwa kila Programu katika Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**77. Mheshimiwa Spika,** naomba pia nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa maelekezo yake anayotupa katika kutekeleza majukumu yetu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuingoza vema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwaletea wananchi maendeleo hasa katika nyanja

ya kidijitali. Kwa uhakika uongozi wake umeleta maendeleo na mapinduzi makubwa ambayo yanaonesha nia ya dhati ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030. Hivyo, sote tunapaswa kumpongeza na kumshukuru kwa kushiriki katika kutekeleza mipango ya mandeleo tuliyopanga.

78. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu, katika kutekeleza majukumu yake inashirikiana na washirika wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi, katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Sekta ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu. Kwa niaba ya Wizara, kipekee napenda kuchukua fursa hii, kuzitambua, kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi ambazo tumeshirikiana katika kuendeleza Sekta za Wizara hii. Shukurani za dhati ziende kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (ITU), Shirika la Umoja wa Posta Duniani (UPU), Benki ya Dunia (WB), Shirika la Umoja wa Posta Afrika (PAPU), Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), Mfuko wa Maendeleo ya Mtaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF), na Taasisi ya Tony Blair (TBI).

79. **Mheshimiwa Spika,** vilevile napenda kuwashukuru watoa huduma za mawasiliano kutoka katika makampuni ya simu ya Airtel, Vodacom, Viettel (Halotel), Honora (Yas), TTCL, Zanlink na ComNet kwa utoaji na usambazaji wa huduma za mawasiliano nchini. Napenda pia kuzitambua Taasisi za Jumuiya ya Kampuni Chipukizi (ZSA), ZRCP, NMB, CRDB, PBZ, Unique Touch, na TanZenj kwa mchango wao wa kuendeleza na kukuza bunifu za TEHAMA nchini. Aidha, natambua mchango wa Kampuni ya Minara Tanzania, Hellios Towers, Towerco of Africa na Raddy Fiber katika kujengea miundombinu ya mawasiliano nchini.

80. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa shughuli

za maendeleo zilizopangwa zinatekelezwa na kuwezesha Sekta ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu inachangia katika kutimiza malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050. Aidha, kwa niaba ya Serikali na kwa kupitia Baraza lako tukufu naomba kutoa wito, kuwaomba wadau waliotajwa hapo juu na wengineo kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutoa huduma za Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

81. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu, imeendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Taasisi zake katika utoaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu. Taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambazo zimekua zikishirikiana na Wizara kwa karibu katika utekelezaji wa majukumu yake ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Shirika la Posta Tanzania (TPC), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Tume ya TEHAMA (ICTC) na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC).

82. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati Viongozi wa Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu, nikianza na Mheshimiwa Mohamed Sijamin Mohamed, Naibu Waziri ambaye pia ni Mwakilishi wa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Kwahani. Aidha, niwapongeze Wenyeviti wa Bodi za Shirika la Mawasiliano Zanzibar na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar, Katibu Mkuu Ndugu Fatma Mabrouk Khamis, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Hawwah Ibrahim Mbaye, Kaimu Afisa Mdhamini Ndugu Ibrahim Saleh Juma, Mkurugenzi Idara ya Uendeshaji na Utumishi Ndugu Saada Ali Mohammed, Mkurugenzi Idara ya Mipango Sera na Utafiti Ndugu Abubakar Ali Sheha, Mkurugenzi Idara ya Mawasiliano na Miundombinu

Ndugu Issa Hamad Bakar, Mkurugenzi Idara ya Usalama Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Mhandisi Khalfan Mohamed Othman, Mkurugenzi Idara ya Ubunifu Ndugu Samora John Chacha, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Mawasiliano Zanzibar Mhandisi Shukuru Awadh Suleiman na Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar Dkt. Said Seif Said. Aidha, napenda kuwashukuru Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Divisheni na Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kutekeleza majukumu yao kwa bidii, weledi na ufanisi.

**Hitimisho**

**83. Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia hotuba ya makadirio ya bajeti kwa mwaka 2026/2027 kwa mara nyengine tena naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano, Ardhi na TEHAMA kwa namna inavyoisaidia Wizara yetu katika utekelezaji wa majukumu yake. Wizara itaendelea kufanyakazi na Kamati hii kwa ukaribu zaidi katika kuwatumikia wananchi kuleta mageuzi ya kidijitali.

**84. Mheshimiwa Spika,** ili Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu iweze kutekeleza kazi zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 naliomba Baraza lako kuidhinisha Jumla ya **Shilingi 53,391,800,000** kati ya Fedha hizo **Shilingi 12,026,800,000** kwa ajili ya matumizi ya Kazi za Kawaida na Mshahara na **Shilingi 41,365,000,000** kwa kazi za Maendeleo.

**85. Mheshimiwa Spika,** Naomba Kutoa Hoja.



**MHESHIMIWA MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM),**
**WAZIRI WA MAWASILIANO, TEKNOLOJIA YA HABARI**
**NA UBUNIFU.**

# VIAMBATISHO

## G. VIAMBATISHO

**Kiambatisho Nambari 1 A: Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Kwa Programu Kwa Kipindi cha Julai, 2026 hadi Machi, 2026.**

| Nam. | FUNGU | KILICHOPANGWA ROBO TATU (JULAI 2025 - MACHI 2026) | | | KILICHOPATIKANA ROBO TATU (JULAI 2025-MACHI 2026) | | | % YA MSHAHARA | % YA OC | ASILIMIA YA JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MSHAHARA | OC | JUMLA | MSHAHARA | OC | JUMLA | | | |
| 1 | Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu | 284,935,500 | 545,961,394 | **830,896,894** | 216,394,950 | 584,425,319 | **800,820,269** | **76** | **107** | **96** |
| 2 | Miradi ya Maendeleo | | 61,650,900,000 | **61,650,900,000** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **JUMLA** | | | **62,481,796,894** | | | **800,820,269** | | | **1.3** |

**Kiambatisho Nambari 1 B: Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Kwa Programu Kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026.**

| Na m. | FUNGU | KILICHOPANGWA ROBO TATU (JULAI 2025- MACHI 2026) | | | KILICHOPATIKANA ROBO TATU (JULAI 2025-MACHI 2026 ) | | | ASILIMIA YA MSHAHARA | ASILIMIA YA OC | ASILIMIA YA JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MSHAHARA | OC | JUMLA | MSHAHARA | OC | JUMLA | | | |
| 1 | Mamlaka ya Serikali Mtan | 1,147,350,849 | 2,008,140,330 | **3,155,491,179** | 1,111,562,868 | 1,173,532,669 | **2,285,095,537** | 97 | 58 | 72 |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | dao-Unguja | | | | | | | | | |
| 2 | Uratibu wa Serikali Mtandao-Pemba | 297,054,604 | 213,368,760 | **510,423,364** | 304,353,475 | 108,823,417 | **413,176,892** | 102 | 51 | 81 |
| | **JUMLA** | **1,444,405,453** | **2,221,509,090** | **3,665,914,543** | **1,415,916,343** | **1,282,356,086** | **2,698,272,429** | **98** | **58** | **74** |

**Kiambatisho Namabari 2: Orodha ya Maeneo na Kampuni zilizojenga Minara**

| Na | Eneo | Mkoa | Wilaya | Kampuni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mwera Minanasini | Mjini Magharibi | Magharibi A | Halotel |
| 2. | Chuini | | | |
| 3. | Kijichi | | | |
| 4. | Fuoni Uwandani | | Magahribi B | |
| 5. | Kitope Skuli | Kaskazini Unguja | Kaskazini B | |
| 6. | Makunduchi | Kusini Unguja | Kusini | |
| 7. | Mwembemakumbi | Mjini Magharibi | Mjini | Towerco of Africa Tanzania Limited (TOA) |
| 8. | Nyarugusu | | Magharibi B | |
| 9. | Kisauni | | | |
| 10. | Shakani | | | |
| 11. | Bambi | Kusini Unguja | Kati | |
| 12. | Ziwa Maboga | Mjini Magharibi | Magharibi B | Halotel |
| 13. | Jumbi | | | |
| 14. | Mwera Pongwe | | Magharibi A | |
| 15. | Jambiani | Kusini Unguja | Kusini | |
| 16. | Cheju | | Kati | |
| 17. | Mpapa | | | |

| Na | Eneo | Mkoa | Wilaya | Kampuni |
|---|---|---|---|---|
| 18. | Chamanangwe Kiuyu | Kaskazini Pemba | Wete | |
| 19. | Wingwi Mapofu | | Micheweni | |
| 20. | Kojani | | Wete | |
| 21. | Micheweni Shanake | | Micheweni | |
| 22. | Kangani | Kusini Pemba | Mkoani | |
| 23. | Vungwi Mafufuni | Kaskazini Unguja | Kaskazini B | Towerco of Africa (TOA) |
| 24. | Cheju Kisomanga | Kusini Unguja | Kati | |
| 25. | Pongwe Kati | | | |
| 26. | Mtule | | Kusini | |
| 27. | Sunrise Dongwe | | | |

**Kimbatanisho Nambari 3: Minara ya Simu kwa aina ya teknoljia ya urushaji wa mawimbi (2G, 3G, 4G na 5G) kwa mikoa ya Zanzibar**

| NA | MKOA | 2G | 3G | 4G | 5G | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kaskazini Pemba | 67 | 65 | 62 | 3 | **197** |
| 2 | Kaskazini Unguja | 97 | 92 | 95 | 5 | **289** |
| 3 | Kusini Pemba | 73 | 72 | 71 | 4 | **220** |
| 4 | Kusini Unguja | 109 | 105 | 110 | 8 | **332** |
| 5 | Mjini Magharibi | 267 | 271 | 276 | 95 | **909** |
| | **JUMLA** | **613** | **605** | **614** | **115** | **1947** |

**Kiambatisho Nambari 4: Mgawanyo wa Minara ya Simu kwa Kila Mkoa**

| NA | MKOA | IDADI YA MINARA MACHI, 2025 | IDADI YA MINARA DISEMBA, 2025 |
|---|---|---|---|
| 1 | Kaskazini Pemba | 61 | 59 |
| 2 | Kaskazini Unguja | 38 | 45 |
| 3 | Kusini Pemba | 56 | 60 |
| 4 | Kusini Unguja | 38 | 63 |
| 5 | Mjini Magharibi | 235 | 228 |
| | **JUMLA** | **428** | **455** |

**Kiambatisho Nambari 5: Idadi ya laini za simu kwa Mikoa ya Zanzibar**

| NA | MKOA | IDADI YA LAINI ZA SIMU MACHI, 2025 | IDADI YA LAINI ZA SIMU MACHI, 2026 |
|---|---|---|---|
| 1 | Kaskazini Pemba | 139,703 | 172,982 |
| 2 | Kaskazini Unguja | 82,625 | 102,308 |
| 3 | Kusini Pemba | 139,465 | 172,687 |
| 4 | Kusini Unguja | 124,337 | 153,955 |
| 5 | Mjini Magharibi | 572,386 | 708,736 |
| | **JUMLA** | **1,058,516** | **1,310,668** |

**Kiambatisho Nambari 6: Kuunganisha Taasisi za Umma na Mtandao wa Serikali (Government Network Connectivity)**

| SEHEMU YA VITUO | VITUO | VIMEFIKISHWA MKONGA (FIBER) | VILIVYOWEKEWA VIFAA VYA KUUNGANISHA HUDUMA YA INTERNET | VILIVYO UNGANISHWA NA HUDUMA YA INTANETI | VITUO VILIVYOKUA BADO HAVIJAPELEKEWA MKONGA |
|---|---|---|---|---|---|
| UNGUJA | 134 | 101 | 95 | 40 | 33 |
| PEMBA | 77 | 52 | 52 | 0 | 25 |
| **JUMLA** | **211** | **153** | **147** | **40** | **58** |

**Kiambatisho Nambari 7: Mgawanyiko wa Mapato ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2026/2027.**

| **Namba** | **Chanzo cha Mapato** | **Makisio ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2026/2027** |
|---|---|---|
| 1. | Mapato yatokanayo na matumizi ya Mkonga wa Mawasiliano (Capacity lease) | 13,291,480,000 |
| 2. | Mapato yatokanayo na Huduma za Mtandao (Internet) | 1,800,000,000 |
| 3. | Mapato yatokanaya na huduma zinazotolewa na Data Center | 1,043,520,000 |
| 4. | Mapato yatokanayo na Tozo za Minara (Tower Leavy) | 865,000,000 |
| **JUMLA KUU** | | **17,000,000,000** |

**Kiambatisho Nambari 8: Mchanganuo wa fedha za Matumizi ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2026/2027.**

| Namba | MAKISIO HUSIKA | KIWANGO KILICHOTENGWA |
|---|---|---|
| 1. | Mshahara | 2,700,000,000 |
| 2. | Kazi za Kawaida | 9,638,668,671 |
| 3. | Miradi ya Maendeleo | 33,365,000,000 |
| **Jumla Ya Fedha** | | **45,703,668,671** |